**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI**
**IDARA YA UHAMIAJI**

*Tarehe:: 30 Januari, 2026*

# TAARIFA KWA UMMA

## KUHUSU KUTOKUWEPO HEWANI KWA MUDA MFUMO WA UTOAJI HUDUMA YA VISA KWA NJIA YA MTANDAO (*ONLINE VISA*)

Idara ya Uhamiaji inapenda kuwajulisha wananchi, wageni na wadau kuwa inafanya maboresho ya mfumo wa utoaji huduma ya Visa kwa njia ya mtandao ***(online Visa)*** ili kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma hiyo kwa wageni wanaotarajia kuja nchini kwa madhumuni mbalimbali.

Zoezi hilo limepangwa kufanyika tarehe 31 Januari, 2026 kuanzia saa 12:00 jioni hadi tarehe 01 Februari, 2026 saa 04:00 asubuhi. Wakati wa maboresho hayo wageni ambao hawana visa watapata visa wakati wa kuingia nchini (*visa on arrival*), wageni ambao wana visa hai wataruhusiwa kuingia nchini (bila kuathiri Sheria ya Uhamiaji, Sura ya 54 na Kanuni za Visa za Mwaka 2016).

Idara ya Uhamiaji inaomba radhi kwa usumbufu wowote utakaojitokeza katika kipindi chote cha maboresho hayo.

**Imetolewa na**

SSI. Paul J. Mselle
**MSEMAJI WA IDARA YA UHAMIAJI**

Ofisi ya Kamishna Jenerali wa Uhamiaji, Eneo la Uzunguni, 4 Barabara ya Mwangosi, S. L. P. 1181,Dodoma.
Simu: +255 262323542/+255 262323543, Nukushi: +255 262323532
Barua pepe: info@immigration.go.tz Tovuti: www.immigration.go.tz
Uhamiaji Tanzania